JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI

# MUHTASARI WA MKAKATI WA TAIFA WA MATUMIZI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

(2024 – 2034)

MEI, 2024



# MUHTASARI RASMI



Sekta ya Nishati Tanzania inachangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi na maendeleo ya nchi. Takribani asilimia 72.5 ya nishati hutumika majumbani kwa shughuli mbalimbali ikiwemo kupika. Upishi ni moja ya shughuli ambazo hufanyika katika kila kaya hivyo kuifanya Serikali kuwa na jitihada za makusudi kuhakikisha kazi ya upishi inafanyika kwa urahisi na usalama kwa kuongeza matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Kwa muktadha wa Tanzania, nishati safi ya kupikia inajumuisha nishati na teknolojia ambapo kwa pamoja hutoa moshi wenye kiwango kidogo cha sumu pale zinapotumika kwa usahihi. Aidha, nishati safi ya kupikia inapaswa kuwa na ufanisi, yenye unafuu, salama na inayopatikana kwa urahisi. Hata hivyo, takwimu zinaonesha kuwa asilimia 6.9 tu ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia, kiasi ambacho ni chini ya wastani wa kiwango cha dunia cha asilimia 71. Matumizi ya nishati isiyo safi ya kupikia yameendelea kuongezeka ambapo asilimia 90 ya kaya hutumia nishati ya kuni na mkaa kama nishati kuu ya kupikia.

Matumizi ya nishati isiyo safi ya kupikia yana athari mbalimbali za kiafya zinazosababisha kudhoofika kwa mfumo wa upumuaji, athari za kimazingira zinazotokana na uharibifu na upotevu wa misitu zinazochangiwa na ukataji wa miti kwa ajili ya kuni na mkaa, athari za kijamii kama vile ukatili wa kijinsia, athari za kielimu na kiuchumi kutokana na muda mwingi kutumika kutafuta nishati hizo.



Pamoja na juhudi za wadau mbalimbali katika kuongeza matumizi ya nishati safi ya kupikia, kumekuwa na changamoto ya kuziunganisha na kupata matokeo yenye tija katika ngazi ya kitaifa. Hivyo, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeandaa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia wa Mwaka



2024-2034 ambao unalenga kuongeza matumizi ya nishati safi ya kupikia kufikia asilimia 80 ya Watanzania wanaotumia nishati hiyo.

Mkakati huu umeandaliwa kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo ya kitaifa na kimataifa inayohusika na nishati safi ya kupikia ikiwemo Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ya Mwaka 2030 (SDGs, 2030), Ajenda ya Umoja wa Afrika 2063, Ajenda ya Tanzania ya Nishati Endelevu kwa Wote (SEforALL 2015) na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025.

## DIRA YA MKAKATI

Kila Mtanzania atumie nishati safi ya kupikia ili kulinda afya, mazingira na kuboresha maisha.

## DHIMA YA MKAKATI

Kuhakikisha upatikanaji wa nishati safi ya kupikia iliyo nafuu, endelevu, salama na rahisi kutumika.

Serikali ya Tanzania imejipanga kutekeleza Mkakati huu kwa kupitia malengo mahususi ambayo yanalenga kutatua changamoto mbalimbali zinazoweka vikwazo katika matumizi ya nishati safi ya kupikia.

# Malengo mahususi ya Mkakati huu ni kama ifuatavyo

### i Kuongeza uelewa wa wananchi na taasisi kuhusu umuhimu wa matumizi ya nishati safi ya kupikia

kupitia programu mbalimbali za uelimishaji na uhamasishaji ili kuondoa fikra hasi zinazosababisha ukinzani kwa matumizi ya nishati hizo. Hii itahusisha mijadala ya kitaifa, majukwaa yenye ushawishi, pamoja na elimu kuanzia ngazi ya chini ya kijamii.

### ii Kuimarisha upatikanaji wa malighafi na miundombinu ya nishati safi ya kupikia

kwa kushirikiana na sekta binafsi katika uzalishaji, upokeaji, uhifadhi na usambazaji wa nishati safi ya kupikia. Hii itahusisha uandaaji wa mitambo ya mfano, ugawaji wa maeneo maalumu kwa ajili ya usambazaji wa nishati safi ya kupikia pamoja na kutumia malighafi zinazopatikana katika maeneo yanayotuzunguka.

### iii Kupunguza gharama za nishati safi, vifaa na majiko sanifu ya kupikia

kwa kupunguza tozo na kodi zinazotozwa katika nishati, vifaa na majiko sanifu ya nishati safi ya kupikia, kutoa ruzuku na kubuni mifumo ya kifedha na teknolojia ya kuwezesha watumiaji kumudu gharama za nishati hiyo kwa kuzingatia kipato chao.

### iv Kuandaa, kuoanisha na kuhuisha Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo wezeshi itakayofanikisha matumizi ya nishati safi ya kupikia

kwa kuandaa miongozo ya viwango vya ubora wa nishati, vifaa na majiko ya kupikia, kuweka mifumo na kanuni za usimamizi wa mnyororo wa thamani wa nishati safi ya kupikia, pamoja na kujumuisha masuala ya nishati safi ya kupikia katika mipango ya matumizi ya ardhi na ujenzi wa majengo ya makazi na biashara.

Vilevile, itahusisha uandaaji wa Mfuko maalumu wa kutekeleza majukumu ya nishati safi ya kupikia, kuwepo kwa katazo la matumizi ya kuni na mkaa kwa taasisi za umma na binafsi pamoja na kuwepo kwa maafisa dawati wa nishati safi ya kupikia kwa ajili ya kuratibu utekelezaji wa mkakati Serikalini.

### v Kuhamasisha uwekezaji katika nishati safi ya kupikia

kwa kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kutumia fursa za biashara zilizopo katika mnyororo wa thamani wa nishati safi ya kupikia, na kuhamasisha matumizi ya mifuko ya fedha na programu za kitaifa katika kukuza na kuendeleza uwekezaji nchini. Jitihada hizi zinajumuisha uandaaji wa kanzidata ya takwimu na taarifa kuhusu nishati safi ya kupikia, mikopo yenye riba nafuu na kuhamasisha biashara ya kaboni katika miradi ya nishati safi ya kupikia.

## vi Kujenga uwezo wa watekelezaji wa miradi ya nishati safi ya kupikia

kwa kutoa elimu ya ufundi na mafunzo stadi kuhusu nishati safi ya kupikia, kutoa elimu na kufunga miundombinu ya kupima viwango vya ubora wa nishati, vifaa na majiko ya nishati safi ya kupikia, mafunzo kwa wajasiriamali kuhusu nishati safi ya kupikia na kuzingatia ushiriki wa wazawa katika miradi ya nishati safi ya kupikia. Vilevile, kujumuisha masuala ya nishati safi katika mitaala ya kufundishia shuleni ili kujenga kizazi chenye uelewa. Aidha, utendaji kazi wa idara ya usimamizi wa biashara ya kaboni utaimarishwa kupitia mafunzo mbalimbali.

## vii Kuongeza wigo wa tafiti na ubunifu wa teknolojia zinazohusu nishati ya kupikia

kwa kuimarisha ushirikiano kati ya wawekezaji wa nishati safi ya kupikia na Taasisi za utafiti na maendeleo pamoja na kutoa mafunzo kwa wakufunzi. Pia, kutenga bajeti katika uendelezaji wa tafiti, ubunifu na uvumbuzi wa teknolojia zinazohusu nishati safi ya kupikia.

## viii Kujumuisha masuala ya usawa wa kijinsia katika masuala ya nishati safi ya kupikia

kwa kuhamasisha ushiriki wa wanawake na vijana katika mnyororo wa thamani wa nishati safi ya kupikia kwa kupitia programu mbalimbali. Vilevile, kuhakikisha usawa wa kijinsia katika ngazi za uamuzi katika masuala yanayohusu nishati safi ya kupikia kwa kutoa mafunzo mbalimbali ya uongozi.

Mkakati huu unatekelezwa na wadau mbalimbali ikiwemo Wizara, Taasisi za Umma, Idara za Serikali, Tawala za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Asasi za Kiraia, Sekta Binafsi, Washirika wa Maendeleo na Umma kwa ujumla. Utekelezaji wa Mkakati huu upo chini ya usimamizi wa Wizara ya Nishati na uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Gharama ya kutekeleza mkakati huu katika kipindi cha miaka 10 ni takriban Shilingi Trilioni 4.6 (Dola za Kimarekani Bilioni 1.8).

Mfumo ya ufuatiliaji na tathmini umeandaliwa ili kuhakikisha Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia unatekelezwa kwa ufanisi na malengo yake yanafikiwa kwa wakati kama ilivyokusudiwa. Mfumo huu pia utasimamia na kutoa mwongozo wa ushiriki wa watendaji katika utekelezaji na ufuatiliaji; kudhibiti na kupima matumizi ya rasilimali wakati wa utekelezaji wa Mkakati; na kupima wajibu wa kila mdau na jinsi alivyowajibika katika utekelezaji